JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

(MAENDELEO YA JAMII)

MWONGOZO WA UANZISHWAJI, UENDESHAJI NA UFUATILIAJI WA DAWATI LA JINSIA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NA ELIMU YA KATI

AGOSTI, 2021

YALIYOMO

YALIYOMO i

UFUPISHO WA MANENO iii

UFAFANUZI WA ISTILAHI iv

DIBAJI vi

SURA YA KWANZA 1

UTANGULIZI 1

1.1 Maelezo ya Awali 1

1.2 Lengo Kuu la Mwongozo 2

1.3 Malengo Mahsusi ya Mwongozo 2

1.4 Umuhimu wa Mwongozo 2

1.5 Walengwa wa Mwongozo 3

1.6 Wigo wa matumizi ya Mwongozo 3

SURA YA PILI 4

CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA WA MWONGOZO 4

2.1 Chimbuko la Mwongozo 4

2.2 Msingi wa Kisheria 4

SURA YA TATU 6

MUUNDO NA MAJUKUMU YA DAWATI LA JINSIA 6

3.1 Muundo wa Dawati la Jinsia 6

3.2 Uteuzi wa Mratibu na Wajumbe wa Dawati 6

3.4 Majukumu ya Dawati la Jinsia 7

3.5 Uendeshaji wa Dawati la Jinsia 8

3.6 Majukumu ya Mratibu wa Dawati la Jinsia 9

3.7 Utoaji wa Taarifa za Ukatili wa Kijinsia 9
3.8 Ulinzi wa Mhanga na Mlalamikiwa wa Ukatili wa Kijinsia 10
3.9 Maeneo ya Rufaa 10
SURA YA NNE 11
MAJUKUMU YA WIZARA, TAASISI NA WADAU 11
4.1 Utangulizi 11
4.2 Wizara yenye dhamana ya kuratibu masuala ya Jinsia 11
4.3 Majukumu ya Wizara zenye Taasisi 11
4.4 Wajibu wa Wakuu wa Taasisi 12
4.5 Wathibiti Ubora 12
SURA YA TANO 13
UFUATILIAJI NA TATHMINI 13
5.1 Utangulizi 13
5.2 Ufuatiliaji 13
5.3 Tathmini 14
5.4 Hitimisho 14

UFUPISHO WA MANENO

AZAKI	Asasi za Kiraia
CCM	Chama Cha Mapinduzi
IRDP	Institute of Rural Development Planning (Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini)
LSF	Legal Service Facility (Shirika linaloshughulikia Huduma za Kisheria)
MTAKUWWA	Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto
NACTE	National Council for Technical Education (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi)
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TCU	Tanzania Commission for Universities (Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania)
UNFPA	United Nations Population Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu)
WAMJW	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
WiLDAF-Tanzania	Women in Law and Development in Africa -Tanzania (Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika)

UFAFANUZI WA ISTILAHI

(Ufafanuzi wa Istilahi hizi unaendana na Matumizi ya Madhumuni ya Mwongozo huu):

“Dawati la Jinsia” ni kitengo/Ofisi maalum katika Taasisi ya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kilichoundwa/iliyoundwa Kushughulikia na Kuimarisha Mfumo wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia

Elimu ya Juu ni elimu ya Stashahada ya Juu, Shahada, stashada ya Uzamili, Shahada ya Uzamili/Umahili na Shahada ya Uzamivu zinazotolewa na Taasisi zilizothibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi/Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania.

Elimu ya Kati ni elimu ya Astashahada na Stashahada zinazotolewa na Taasisi zilizothibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Jinsi ni hali ya kibaolojia inayombainisha mtu kuwa wa kike au wa kiume.

Jinsia ni dhana inayoonyesha mahusiano yanayojengwa na jamii ili kutofautisha kati ya wanaume na wanawake ambapo mahusiano hayo yanagawa majukumu na wajibu tofauti kwa kila jinsi kutegemeana na utamaduni, mila na desturi.

Taasisi Binafsi ni Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Mashirika ya Dini, Mashirika yasiyo ya Kidini au Watu binafsi.

Taasisi za Umma ni Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Serikali.

Taasisi ni Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

Ukatili ni kitendo chochote chenye kuleta madhara anachofanyiwa mwanamke/mwanaume na kumuathiri/kuwaathiri kimwili, kiuchumi, kiakili au kisaikolojia.

Ukatili wa Kijinsia ni kitendo chochote anachofanyiwa mtu/watu kinachoweza kusababisha madhara ya kimwili, kiakili, kisaikolojia, au mateso mengine.

Usawa wa Jinsia Uwepo wa haki na fursa sawa kwa jinsi zote kushirikishwa kwa usawa bila kujali Jinsi.

Wadau ni Wizara, Idara, Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati za Umma, Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati za Binafsi na AZAKI zinazohusika katika Mwongozo huu.

Wathibiti Ubora ni vyombo vinavyohusika na kudhibiti ubora wa elimu katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ambavyo ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)

Wakuu wa Taasisi ni Makamu wa Wakuu wa Vyuo Vikuu na Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Kati.

Watoa huduma ni Kampuni au watu binafsi wanaoendesha shughuli mbalimbali ndani ya Taasisi kama vile:- malazi, usafi, ulinzi, usafiri, chakula, machapisho ambao siyo Wafanyakazi wa Taasisi husika.

Wigo ni maeneo ambayo Mwongozo unatumika.

Wizara yenye dhamana na Masuala ya Jinsia ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

DIBAJI

Serikali ya Tanzania imefanya jitihada mbalimbali katika kutokomeza ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018-2021/2022. Mwongozo huu ni moja ya jitihada za Serikali za kutokomeza ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Aidha, Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo ya uanzishwaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

Kupitia Mwongozo huu, Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati zinatarajiwa kutoa kipaumbele katika masuala ya kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kutoa taarifa zenye takwimu zilizoainishwa kijinsia na kuweka mipango mahsusi ya kuondoa tofauti za kijinsia. Malengo haya yatafikiwa iwapo kila Taasisi itaanzisha Dawati la Jinsia litakaloshughulikia ajenda za masuala ya kijinsia na ukatili wa kijinsia pamoja na kuweka juhudi za kuelimisha Wanafunzi, Wafanyakazi pamoja na watoa huduma katika maeneo ya Taasisi kuhusu umuhimu wa kuzingatia masuala ya kijinsia katika shughuli zao za kila siku.

Hivyo basi, kila Taasisi haina budi kujiwekea utaratibu wa kupanga mipango na bajeti yenye kuzingatia mahitaji ya kijinsia. Hatua hii itawezesha kila kundi katika Taasisi kufikiwa kwa kuzingatia mahitaji yao ya kijinsia. Pia, itasaidia Taasisi kuwa na mipango inayotekelezeka na endelevu ili kila kundi liweze kunufaika na mipango ya Taasisi husika.

Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kuzielekeza Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kuanzisha Dawati la Jinsia ili kuziwezesha Taasisi hizo kupanga na kutekeleza mipango madhubuti yenye kuzingatia mahitaji, vipaumbele na fursa za kijinsia ili kutokomeza aina zote za ukatili na hatimaye kufikia usawa wa kijinsia. Hatua hii, itawezesha kuandaa kizazi cha wanafunzi kinachofanya kazi kwa kujiamini, kujituma na kujitegemea katika mazingira mbalimbali ambayo wahitimu wataitumikia jamii na Taifa kwa ujumla.

Hivyo,tunatarajia kuwa Wizara, Idara na Taasisi zenye vyuo vilivyo chini yake, Mashirika na Wadau wa Maendeleo wanaohusika na Mwongozo huu kuutumia kikamilifu kwa ajili

ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kuzuia na kutokomeza vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Taasisi. Aidha, Utekelezaji wa Mwongozo huu utawezesha Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kutoa elimu katika mazingira bora na salama.

Kukamilika kwa Mwongozo huu ni matokeo ya juhudi za pamoja za Wadau mbalimbali walioshiriki kwa namna moja au nyingine. Hivyo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Jamii inatoa shukrani za dhati kwa Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi waliowezesha mwongozo huu kukamilika ambazo ni Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Kilimo; Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE); Jeshi la Polisi Tanzania; Jeshi la Magereza Tanzania; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati hapa nchini.

Pia, tunapenda kutoa shukrani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF-Tanzania) kwa michango yao ya fedha na utaalam ambao umewezesha kukamilika kwa Mwongozo huu.

Dkt.John. K. Jingu
KATIBU MKUU

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na kusimamia uingizwaji na utekelezaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango, Programu, Miongozo, Mikakati, na Bajeti zinazotekelezwa hapa Nchini. Uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia katika Sekta za Umma na Sekta Binafsi ni sehemu ya utekelezaji na uzingatiaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 pamoja na Mkakati wa utekelezaji wake wa mwaka 2005.

Vilevile, Wizara inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 – 2021/22, ambapo moja ya maeneo nane (8) ya kimkakati katika utekelezaji wa Mpango huu ni mwitikio na huduma saidizi kwa waathirika wa vitendo vya ukatili ambapo Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ni wahusika mahsusi katika utekelezaji wa eneo hili.

Baadhi ya Mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuwepo kwa Mpango Kazi huo ni pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa Jamii ya Tanzania kuhusiana na masuala ya ukatili wa kijinsia na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa vyombo husika ambapo katika mwaka wa Fedha 2020/21 jumla ya matukio 20,025 ya ukatili yalipokelewa ikilinganishwa na matukio 18,270 yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuanzishwa kwa Madawati ya Polisi ya Jinsia na Watoto 420; kuanzishwa kwa Kamati za ulinzi wa Wanawake na Watoto 18,186 ; kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijiji/Mtaa; na kuanzishwa kwa vituo vya mkono kwa mkono 14 katika Hospitali za Serikali.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo bado kuna matukio ya vitendo na viashiria vya ukatili wa kijinsia vinaendelea kuongezeka hususan katika maeneo ya Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Katika kushughulikia changamoto hiyo tarehe 23 Desemba 2019, Serikali kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya

Maendeleo ya Jamii), ilifanya mkutano na wawakilishi wa Wakuu wa Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kwa ajili ya kujadili namna bora ya kushughulikia ukatili wa kijinsia. Mkutano huo uliazimia kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na kati ili kutokomeza ukatili wa kijinsia na kukuza Usawa wa Jinsia.

1.2 Lengo Kuu la Mwongozo

Kuweka mfumo wa pamoja wa uanzishwaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia na uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya maendeleo ya Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati

1.3 Malengo Mahsusi ya Mwongozo

i. Kuelekeza Taasisi kuandaa na kuanzisha Dawati la Jinsia litakaloshughulikia uingizwaji wa masuala ya kijinsia na ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi;
ii. Kuelekeza muundo na majukumu ya Dawati la Jinsia kwenye Taasisi husika;
iii. Taasisi kuandaa na kutekeleza mkakati wa kushughulikia na kutokomeza ukatili wa kijinsia;
iv. Kuelekeza kila Taasisi ya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kuteua Mratibu wa Dawati la Jinsia; na
v. Kuelekeza Taasisi kutenga rasilimali fedha na vifaa kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya uendeshaji wa Dawati la Jinsia;

1.4 Umuhimu wa Mwongozo

i. Kuwezesha uanzishwaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati;
ii. Kuainisha muundo na Majukumu ya Dawati la Jinsia kwenye Taasisi;
iii. Kuwezesha kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Taasisi litakalosimamia na kushughulikia vitendo vya ukatili wa kijinsia;
iv. Kuwezesha kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Taasisi litakalosimamia uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango na bajeti za kila mwaka;
v. Kuwezesha kueleweka kwa masuala ya ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

1.5 Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu umelenga kutumiwa na:

i. Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali zinazosimamia Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati zilizo chini yao:-
ii. Wathibiti Ubora katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati kama vile Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na Wadau wengine wanaoshirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.
iii. Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati;
iv. Waratibu wa Dawati la Jinsia;
v. Wafanyakazi wanaofanya kazi katika Taasisi;
vi. Wanafunzi na Uongozi wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi husika; na
vii. Watoa huduma katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati;

1.6 Wigo wa matumizi ya Mwongozo

Mwongozo huu utatumika katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati katika Taasisi zote za Umma na Binafsi za Tanzania Bara. Katika Taasisi hizo Mwongozo huu, utatumiwa na Wahadhiri/Wakufunzi, Wafanyakazi, Wanafunzi na Watoa Huduma kufahamu jinsi ya kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili katika mazingira ya Taasisi husika. Aidha, Mwongozo utatumiwa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali wanaoshughulika na masuala ya kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili wa Kijinsia katika Taasisi.

SURA YA PILI

CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA WA MWONGOZO

2.1 Chimbuko la Mwongozo

Chimbuko la Mwongozo huu limetokana na kuwepo kwa taarifa za matukio na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Kikao kati ya Wizara na Wakuu wa Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati kilichofanyika tarehe 23 Desemba, 2019 katika Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Kampasi Kuu ya Dodoma kwa ajili ya kujadili namna ya kutatua changamoto za vitendo va Ukatili maeneo ya Vyuoni kiliazimia kuandaliwa kwa Mwongozo utakaotoa maelekezo ya uanzishwaji na uendeshaji wa dawati la Jinsia.

Aidha, uandaaji wa Mwongozo huu pamoja na mambo mengine ni utekelezaji wa maelekezo ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenye Hotuba aliyoitoa wakati wa akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 Jijini Dodoma ambapo alizielekeza Taasisi za Umma na Binafsi kuhakikisha zinaweka utaratibu unaofaa wa kutokomeza Ukatili kwa wanawake, wasichana, wavulana na watoto.

2.2 Msingi wa Kisheria

Uandaaji wa Mwongozo huu umezingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Sheria, Mipango, Mikakati na maelekezo ya Serikali ambayo Mwongozo huu umezingatia:

i. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 sehemu ya tatu ibara ya 12 na 13;
ii. Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 na Mkakati wa Utekelezaji wake wa mwaka 2005;
iii. Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008;
iv. Sheria ya Ushahidi sura ya 16;
v. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329;
vi. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20;
vii. Sheria ya Mtoto sura ya 13;

viii. Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 – 2021/22;

ix. Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu wa mwaka 2017- 2022;

x. Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025 ibara ya 231 (a),(i) na (l);

xi. Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano waTanzania iliyotolewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, tarehe 13 Novemba 2020, Jijini Dodoma; na

xii. Hotuba ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 Jijini Dodoma.

SURA YA TATU

MUUNDO NA MAJUKUMU YA DAWATI LA JINSIA

3.1 Muundo wa Dawati la Jinsia

Dawati la Jinsia katika Taasisi litaundwa na Mratibu wa Dawati na watendaji wengine wasiopungua watano (5) na wasiozidi (15) kutegemeana na ukubwa wa Taasisi. Miongoni mwa Wajumbe hao, wawili (2) ni lazima wawe wanafunzi. Uteuzi wa wajumbe wa Dawati uzingatie uwakilishi wa Shule/Vitivo/Ndaki na Jinsia. Aidha, Dawati hili litawekwa chini ya Ofisi ya Mkuu wa Taasisi.

3.2 Uteuzi wa Mratibu na Wajumbe wa Dawati

i. Mratibu wa Dawati atateuliwa na Mkuu wa Taasisi miongoni mwa watumishi wa Taasisi;
ii. Watendaji wengine watateuliwa na Mkuu wa Taasisi kutegemeana na ukubwa wa Taasisi kwa kuzingatia uwiano wa jinsi na Kada;
iii. Wajumbe Wanafunzi watateuliwa na Serikali ya Wanafunzi miongoni mwa wanafunzi ambao siyo Viongozi wa Serikali ya wanafunzi;
iv. Muda wa Mratibu na Wajumbe kutumikia nafasi zao ni miaka mitatu (3);
v. Kwa mjumbe ambaye ni Mwanafunzi, atatumikia nafasi hiyo kwa muda wa mwaka mmoja tu na anaweza kuteuliwa tena;
vi. Mratibu wa Dawati na Wajumbe wanaweza kuteuliwa tena baada ya kumaliza muda wao kutegemeana na maamuzi ya Mkuu wa Taasisi atakavyoona inafaa; na
vii. Iwapo mjumbe atapoteza sifa ya kuwa mjumbe kwa sababu ya kifo, ugonjwa wa kudumu au sababu nyingine zinazosababisha ashindwe kutekeleza majukumu yake Mkuu wa Taasisi atateua mtu mwingine kwa mtumishi na kwa upande wa Wanafunzi Serikali ya Wanafunzi itateua mjumbe mwingine.

3.3 Sifa za Mratibu na Watendaji wa Dawati la Jinsia

i. Awe Mfanyakazi mwenye ajira ya kudumu wa Taasisi husika;
ii. Awe na uelewa wa kutosha kuhusu suala ya ukatili wa kijinsia.
iii. Awe na uwezo wa kusimamia haki na usawa;
iv. Awe mwadilifu kwa matendo (mchapakazi, heshima, maadili mema na awe na uwezo wa kutunza siri);
v. Wanafunzi watakaoteuliwa kuwa wajumbe wa Dawati watatakiwa kuwa na muda wa masomo usiopungua mwaka mmoja wakati wa uteuzi.

3.4 Majukumu ya Dawati la Jinsia

Katika kuhakikisha kuwa maeneo ya kazi na kujifunzia yanakuwa rafiki na salama kwa wafanyakazi na wanafunzi pamoja na watoa huduma mbalimbali kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, Dawati la Jinsia litatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kupokea na kushughulikia taarifa zote za ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi;
ii. Kutoa ushauri nasaha na kuwalinda kisaikolojia wahanga wa ukatili wa kijinsia;
iii. Kutekeleza Sera ya Jinsia na kutoa ushauri wa marekebisho ya Sera husika kwa Menejimenti ya Taasisi;
iv. Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa kushirikiana na Wadau;
v. Kufuatilia na kupokea taarifa kuhusu kesi na rufaa mbalimbali zinazohusu ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi;
vi. Kufuatilia na kupokea taarifa kutoka taasisi na Idara mbalimbali zinazoshughulikia ukatili wa kijinsia;
vii. Kubuni mfumo rafiki na salama wa utoaji wa taarifa za matukio ya Vitendo vya ukatili;
viii. Kushauri Menejimenti kuhusu uzingatiaji na utekelezaji wa masuala ya kijinsia kwenye Sera, Mipango, Programu, Mikakati, Miongozo na Bajeti za Taasisi;
ix. Kuelimisha Jamii ya Taasisi husika kuhusu Ukatili wa Kijinsia pamoja na kuzingatia masuala mbalimbali ya kijinsia katika utekelezaji wa majukumu na wajibu wao;

x. Kufanya tathmini za utekelezaji wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika Taasisi husika na kuchochea kufanyika kwa tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi ndani na nje ya Taasisi;

xi. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za masuala ya kijinsia yanayoripotiwa kwenye Dawati;

xii. Kutoa ushauri nasihi kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia wanaoripoti kwenye dawati;

xiii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za kila robo mwaka (Kila baada ya miezi mitatu); kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Dawati pamoja na utekelezaji wa Mpango kazi wa kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwenye mamlaka ya Taasisi;

xiv. Kuwezesha kuanzishwa klabu za masuala ya jinsia na ukatili wa kijinsia;

xv. Dawati litakuwa na jukumu la kuwaunganisha wahanga wa ukatili wa kijinsia na Ofisi ya Ustawi wa Jamii au vyombo vya kiuchunguzi kama vile TAKUKURU, Dawati la Jinsia na watoto la Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali na vyombo vingine vinavyohusiana na masuala hayo; na

xvi. Wakati uchunguzi wa suala la ukatili wa kijinsia likiendelea, Dawati litawajibika kufuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu za ushahidi kwa ajili ya shauri husika.

3.5 Uendeshaji wa Dawati la Jinsia

Dawati litakuwa linapokea taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia muda wowote kila siku kwa saa ishirini na nne kwa kufuata utaratibu maalum uliopangwa. Aidha, Dawati la Jinsia litakuwa na vikao vya aina tatu ambavyo ni:-

i. Vikao vya Dawati la Jinsia na Menejimenti;

ii. Vikao vya kawaida; na

iii. Vikao vya dharura kulingana na hali halisi ya taarifa zinazoripotiwa.

Vikao vya Dawati vya Kawaida vitafanyika kila robo mwaka. Aidha, Mwanasheria wa Taasisi husika anaweza kualikwa kuhudhuria vikao hivyo endapo itaonekana inafaa.

3.6 Majukumu ya Mratibu wa Dawati la Jinsia

Mratibu wa Dawati la Jinsia atakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Ataripoti kwa Mkuu wa Taasisi husika;
ii. Atakuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Dawati;
iii. Ataingia kwenye vikao vya menejimenti ili aweze kuwasilisha taarifa za ukatili wa kijinsia;
iv. Atatakiwa kuanzisha Club/Vinara wa kuelimisha na kupinga vitendo vya Ukatili kwenye Taasisi;
v. Atakuwa ni mlezi wa klabu za kupinga Ukatili wa kijinsia kwenye Taasisi husika;
vi. Kutoa taarifa ya tukio la dharura kwa Mkuu wa Taasisi wakati wowote;
vii. Kuhakikisha kuwa taarifa za vitendo vya Ukatili wa Kijinsia zinazotolewa kwenye Dawati la Jinsia zinashughulikiwa na kufuatiliwa;
viii. Kuandaa Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia na kusimamia utekelezaji wake kwa kushirikina na Menejimenti, Watendaji wa Dawati na Wadau mbalimbali; na
ix. Mratibu wa Dawati la Jinsia atahudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

3.7 Utoaji wa Taarifa za Ukatili wa Kijinsia

Mtu yeyote anawajibika kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia kwenye Dawati la Jinsia la Taasisi husika. Aidha, Dawati la Jinsia litatakiwa kuandaa utaratibu rafiki wa upokeaji wa taarifa za Ukatili wa Kijinsia ambazo zitafanyika kwa utaratibu ufuatao:-

i. Mfanyakazi, Mwanafunzi, mtoa huduma au mtu yeyote atawajibika kufika kwenye Dawati la Jinsia ili kutoa taarifa kuhusu ukatili au viashiria vya ukatili kwa wakati;
ii. Katika mazingira ambayo Mfanyakazi/Mwanafunzi au Mtoa huduma kwenye Taasisi hawezi kutoa taarifa, ndugu wa karibu/Rafiki/mtu yeyote anaweza kutoa taarifa husika kupitia utaratibu wenye usiri.
iii. Mlalamikaji/Muhanga au mtoa taarifa wa vitendo vya Ukatili wa kijinsia atapaswa kutoa taarifa kwenye dawati kuhusu viashiria vyovyote vinavyohusiana na vitisho au vikwazo atakavyowekewa na mtuhumiwa, marafiki/jamaa wa mtuhumiwa au ndugu wa mtuhumiwa;

iv. Katika mazingira ya utoaji wa haki kwa Mhanga na Mtuhumiwa wa Ukatili wa Kijinsia; taarifa na uchunguzi wa kina zitatakiwa kufanywa ili maamuzi yatakayotolewa yasiache shaka yoyote au kutomtendea haki mtu yeyote; na

v. Taarifa za ukatili wa kijinsia zitapokelewa kwa njia ya mahojiano ya moja kwa moja, barua pepe, ujumbe wa simu, kwa kupiga simu, sanduku la maoni pamoja na taratibu nyingine zitakazowekwa na Taasisi husika kwa ajili ya kupokea taarifa za ukatili wa kijinsia au mtoa taarifa atakavyoona inafaa.

3.8 Ulinzi wa Mhanga na Mlalamikiwa wa Ukatili wa Kijinsia

Katika kipindi chote ambacho Mhanga wa vitendo vya Ukatili wa kijinsia atakapokuwa amewasilisha suala la uwepo wa viashiria vya ukatili au ukatili ambao atakuwa amefanyiwa, Dawati la Jinsia litapaswa kufanya yafuatayo:

i. Kuhakikisha Usalama wa Mlalamikaji, Mhanga, Mlalamikiwa au mtoa taarifa unalindwa kulingana na mifumo ya utendaji na usimamizi iliyopo;

ii. Kuhakikisha utunzaji wa siri unazingatiwa wakati suala au shauri la vitendo vya Ukatili likiendelea na uchunguzi au utaratibu wa kisheria ukiendelea; na

iii. Kuhakikisha mtoa taarifa, Mhanga/Mlalamikaji na Mlalamikiwa/Mtuhumiwa wanalindwa bila kudhurika kwa sababu ya mwenendo wa shauri lao.

3.9 Maeneo ya Rufaa

Baada ya Dawati kupokea taarifa za Ukatili wa kijinsia na endapo shauri litakuwa nje ya uwezo wa Taasisi kisheria, Mratibu anapaswa kutoa rufaa kwa Mhanga kwenda kwenye taasisi husika mfano:-

i. Dawati la Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi;

ii. Taaasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa;

iii. Ofisi za Ustawi wa Jamii;

iv. Vituo vya Mkono kwa Mkono (One Stop Centres);

v. Kituo cha kutolea huduma za Afya ; na

vi. Taasisi za dini.

Tanbihi: Taarifa za vitendo vya Ukatili ziwasilishwe kwenye vyombo/mamlaka yenye uwezo na dhamana ya kushughulikia tatizo husika.

SURA YA NNE

MAJUKUMU YA WIZARA, TAASISI NA WADAU

4.1 Utangulizi

Mwongozo huu umeainisha majukumu ya Wadau wanaojihusisha na uzingatiaji wa masuala ya jinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Wadau wakuu wa Mwongozo huu ni Wizara yenye dhamana ya kuratibu masuala ya jinsia; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama Wizara inayosimamia utoaji wa elimu katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati hapa nchini, pamoja na Wizara zenye Taasisi za Elimu ya Kati na Wathibiti ubora.

4.2 Wizara yenye dhamana ya kuratibu masuala ya Jinsia

Katika kuhakikisha ufanisi wa Madawati yatakayoanzishwa, Wizara yenye dhamana na masuala ya jinsia itatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kuratibu utekelezaji kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya kati;
ii. Kuratibu upokeaji wa taarifa za utekelezaji wa Mwongozo;
iii. Kufanya tathmini ya utendaji wa Dawati kwenye Taasisi;
iv. Kuratibu na kuyajengea uwezo madawati ya Jinsia katika Taasisi;
v. Kuandaa mfumo wa kielekroniki (*Dash board*) kwa ajili ya kukusanya na kutunza taarifa za vitendo vya ukatili kwenye Taasisi.
vi. Kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka zinazotoka kwenye Taasisi na kuzifanyia uchambuzi wa kina.

4.3 Majukumu ya Wizara zenye Taasisi

Majukumu yafuatayo yatahusu Wizara zenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati:

i. Kuteua Afisa atakayeratibu na kusimamia shughuli za Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na elimu ya Kati;
ii. Kupokea taarifa za Robo Mwaka kutoka Taasisi zilizo chini yake na kuziwasilisha katika Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia;
iii. Kufuatilia uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la jinsia katika Taasisi husika; na

iv. Kushiriki katika vikao vitakavyoitishwa kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa Mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati.

4.4 Wajibu wa Wakuu wa Taasisi

Wakuu wa Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati watakuwa na Majukumu yafuatayo ili kuhakikisha kuwa Dawati la Jinsia linatimiza majukumu yake ipasavyo:-

i. Kutenga bajeti za kutosha katika rasilimali watu, fedha na vifaa ili kuwezesha dawati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati;
ii. Kuhakikisha kuwa taarifa za vitendo vya Ukatili wa Kijinsia zinatolewa taarifa kwenye Dawati la Jinsia na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinashughulikiwa;
iii. Kuhakikisha kuwa Wafanyakazi, Wanafunzi na watoa huduma wote wanapata mafunzo kuhusu masuala ya kijinsia;
iv. Kuhimiza na kulielekeza Dawati la Jinsia kutoa taarifa za utekelezaji kwa kila robo mwaka;
v. Kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya Kijinsia katika Taasisi kwa Wizara Husika;
vi. Kuhakikisha kila Taasisi inaandaa na kutekeleza Sera ya Jinsia na mkakati wa utekelezaji wake;
vii. kutoa elimu, ushauri stahiki juu ya masuala ya jinsia na madhara ya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na wadau; na
viii. Kushiriki katika vikao vya tathmini vitakavyoitishwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia kuhusu uendeshaji wa Madawati ya Jinsia.

4.5 Wathibiti Ubora

Wathibiti Ubora wa Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati watakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kuzingatia uwepo wa Dawati la Jinsia katika kila Taasisi kwa ajili ya kushughulikia vitendo vya ukatili wa kijinsia; na
ii. Kuhakikisha suala la Uanzishwaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati linapewa kipaumbele kwa kila Taasisi.

SURA YA TANO

UFUATILIAJI NA TATHMINI

5.1 Utangulizi

Ufuatiliaji, tathmini na taarifa za utekelezaji ni mambo muhimu yanayowezesha Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, Wizara zenye vyuo vilivyo chini yake na Wizara yenye dhamana ya kuratibu masula ya Jinsia kufahamu hali halisi ya utendaji wa Dawati la Jinsia ikiwa ni pamoja na kujua hali ya ukatili wa kijinsia ilivyo kwa kuzingatia Mpango kazi uliopo. Sura hii inatoa ufafanuzi wa namna ya utekelezaji wa mpango kazi kwa kufanya ufuatiliaji, tathmini na uandaaji wa taarifa za utekelezaji.

5.2 Ufuatiliaji

Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu katika Taasisi za elimu ya Juu na Elimu ya Kati kila robo mwaka. Upimaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu utazingatia vipengele vifuatavyo:-

i. Utengaji wa Fedha kwenye Bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya Dawati la Jinsia ndani ya Taasisi;
ii. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Dawati;
iii. Mafunzo ya kuwajengea uwezo Wafanyakazi, Wanafunzi na Wanajumuiya wa Taasisi kuhusu masuala ya Ukatili wa Kijinsia;
iv. Takwimu za matukio yaliyoripotiwa kwenye Dawati la Jinsia kwa uwiano wa Wanawake na Wanaume;
v. Uwepo wa uwezeshaji wa utendaji kazi kwa ajili ya Dawati la Jinsia (mfano mafunzo);
vi. Uwepo wa mifumo ya utoaji wa taarifa mbalimbali za vitendo vya ukatili wa Kijinsia kama vile simu, mifumo ya kielektroniki (dash board) na Sanduku la kutolea maoni; na
vii. Utekelezaji wa Sera ya Jinsia.

5.3 Tathmini

Utekelezaji wa Shughuli za Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, utafanyiwa tathmini kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kupima uingizwaji wa masuala ya jinsia na matokeo ya ushughulikiwaji wa Vitendo vya Ukatili kwenye Taasisi husika.

Mapitio ya Mwongozo yatafanyika kila baada ya miaka mitano (5) au pale itakapoonekana kuna uhitaji au ulazima wa kufanya hivyo. Aidha, Taasisi zitapaswa kujifanyia tathmini kila baada ya mwaka mmoja ili kuona mafanikio na maeneo yanayohitaji kuongeza nguvu.

5.4 Hitimisho

Mwongozo huu ni kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa kushughulikia vitendo vya ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati pamoja na kuzingatia uingizwaji wa masuala ya kijinsia katika Mipango, Bajeti, Mikakati na Programmu za Taasisi. Mwongozo huu utasaidia kuimarisha mahusiano ya kiutendaji na kijinsia kati ya Wahadhiri/Wakufunzi, Wafanyakazi, Wanafunzi na Watoa huduma ndani ya Taasisi ili kwa pamoja waweze kuishi kwenye Taasisi ambayo itakuwa ni sehemu yenye mazingira bora, salama na wezeshi kwa ajili ya utoaji wa elimu hapa nchini.

Mwongozo huu utasaidia kujenga ushirikiano katika utendaji na uratibu wa masuala ya kuzuia ukatili wa kijinsia baina ya Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara zenye Taasisi zilizo chini yake, Taasisi za kiuchunguzi na utoaji maamuzi, Wathibiti Ubora katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati, Wadau wa kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na Waandishi wa habari ili kuwa na kizazi cha usawa wa jinsia kisichokuwa na vitendo vya Ukatili.

Hivyo basi, Wizara inaamini kuwa Mwongozo huu utatumika kama nyenzo na dira muhimu katika kuhakikisha kuwa lengo kuu la Mwongozo ambalo ni kuondoa aina zote za Vitendo vya Ukatili wa kijinsia katika Taasisi ikiwa ni pamoja na uwekaji wa mazingira bora ya utoaji elimu linafikiwa katika kiwango kilichokusudiwa. Aidha, Mwongozo huu utatumika bila kuathiri Sheria, taratibu, kanuni na mifumo ya Serikali iliyopo.